



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI
**WAKALA WA UFUNDI NA UMEME TANZANIA
(TEMESA)**



TAARIFA KWA UMMA

**WITO KWA WAZABUNI WENYE MADAI DHIDI YA TEMESA KUWASILISHA
TAARIFA ZA MADAI YAO**

Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) unapenda kuwataarifu wazabuni wote waliowahi kutoa huduma, bidhaa au kutekeleza kazi mbalimbali kwa Wakala na bado wana madai ambayo hayajalipwa kuwa, wawasilishe taarifa na nyaraka zinazohusu madai hayo kwa ajili ya uhakiki, uthibitisho na uboreshaji wa kumbukumbu za malipo.

Zoezi hili linalenga kuiwezesha TEMESA kuwa na taarifa za madeni yanayodaiwa zilizo kamili, sahihi, na zilizohuishwa ili kurahisisha mchakato wa kuyafanyia kazi kwa kuzingatia taratibu, sheria na kanuni za Serikali.

Wazabuni wote wenye madai wanatakiwa kuwasilisha nyaraka husika, zikiwemo:

- Nakala ya mkataba au oda ya kazi/manunuzi (kama ipo);
- Ankara (Invoice);
- Hati za madai;
- Hati za makabidhiano au uthibitisho wa huduma au kazi iliyotekelezwa;
- Taarifa za akaunti ya benki; na
- Nyaraka nyingine zozote zinazohusiana na madai hayo.

Nyaraka hizo zinaweza kuwasilishwa katika ofisi yoyote ya TEMESA iliyo karibu na mzabuni husika nchini, ndani ya siku thelathini (30) tangu tarehe ya kutolewa kwa taarifa hii.

TEMESA inawahimiza wazabuni wote wenye madai kuitikia wito huu kwa wakati ili kuwezesha zoezi la uhakiki kufanyika kwa ufanisi na kukamilika kwa wakati uliopangwa.

TEMESA inawatakiwa ushirikiano mwema katika utekelezaji wa zoezi hili.

Quality Services for Development Opportunities

**Imetolewa na:
Ofisi ya Mtendaji Mkuu
TEMESA
03/06/2026**

TEMESA HOUSE, 2 Mtaa wa TEMESA 41104 TAMBUKARELI,
S. L. P 1075, Dodoma- Tanzania, Simu: +255 737 962 496, Bila Malipo: 0800110379,
Barua pepe: info@temesa.go.tz, barua@temesa.go.tz, : www.temesa.go.tz

“Huduma Bora Kwa Fursa za Maendeleo”